TANGAZO LA SERIKALI NA. 702 la tarehe 02 /12/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA IGALULA YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Igalula ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa jumla na wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka I1 iliyopo katika makutano ya barabara ya Kigwa na Mto wa msimu wa Igalula Mashariki mwa Shule ya Msingi Isenefu katika majira -nukta 505260E, 9424984N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa bonde la mpunga na kukatisha barabara ya Goweko katika alama ya mpaka I2 yenye majira-nukta 504670E, 9421591N; baada ya hapo mpaka unaendelea Kusini kwa kufuata bonde na kukatiza reli ya Itigi katika alama ya mpaka I3 yenye majira - nukta 504274E, 9419493N; baada ya hapo mpaka utafuata bonde Kusini - Magharibi katika uelekeo wa S105$^{0}$7΄0˝ W kwa umbali wa kilomita 1.06 hadi alama ya mpaka I4 inayopatikana barabara ya Mturu kwa majira - nukta 503182E, 9418943N; baada ya hapo mpaka unaendelea Magharibi - Kaskazini katika uelekeo wa W150$^{0}$10΄0˝N kwa umbali wa kilomita 1.8 hadi alama ya mpaka I5 inayopatikana barabara ya Kawekapina katika majira-nukta 501348E, 9419937N; baada ya hapo mpaka unaendelea kuelekea Magharibi na kukatiza barabara ya Ipululu katika alama ya mpaka I6 yenye majira - nukta 498359E, 9420421N, baada ya hapo mpaka

*Tangazo la Serikali na. 702 (linaendela)*

utaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa $N88^{0}5'52''E$ kwa umbali wa kilomita 2.5 hadi alama ya mpaka I7 yenye majira - nukta 499094E, 9422949N; baada ya hapo mpaka unakatiza reli ya Itigi-Tabora na kuelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa $N175^{0}11'40''$ kwa umbali wa kilomita 4.4 hadi alama ya mpaka I8 iliyopo barabara ya Ndevelwa katika majira - nukta 501140E, 9427337N; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki - Kusini katika uelekeo wa $E155^{0}10'20''$ kwa umbali wa kilomita 4.1 hadi ulipoanzia”.

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*